**HOTUBA YA UFUNGUZI YA MKURUGENZI MKUU WA TUME YA TAIFA YA MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI KATIKA KIKAO CHA KAMATI YA TAIFA YA UFUNDI YA KUSIMAMIA MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI**

**EDEMA - MOROGORO TAREHE 5 HADI 7 SEPTEMBA 2018.**

**Ndugu Wajumbe,**

**Kamati ya Ufundi ya Taifa,**

**Wadau wa washiriki wa Upangaji Matumizi ya Ardhi,**

**Mabibi na Mabwana,**

Napenda kuwakaribisha kwenye kikao chetu cha kurejesha mahali pake kamati ya Taifa ya kiufundi ambayo kwa mara ya mwisho ilifanya kazi ya kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Tume mwaka 2014. Kabla sijaeleza kwanini nimetamka kuwa inarejeshwa, naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu Tume, uanzishwaji wake na majukumu husika,

Tume imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya mwaka 2007 kifungu Na.6. Pia Tume inafanya kazi chini ya Bodi ambayo imeundwa kwa mujIbu wa kifungu Na. 6(1) (a), Mwenyekiti wa Bodi anateuliwa na Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wajumbe wa bodi huteuliwa na Waziri wa Sekta husika na wanatoka katika Sekta za umma na binafsi zinahusika masuala ya uandaajii na usimamizi wa matumizi ya Ardhi.

Kwa kuzingatia Sera ya Ardhi ya mwaka 1995 ambayo inafanyiwa marekebisho na Sera ya Makazi na Nyumba ya mwaka 2002, Tume hutekeleza kazi zake kwa kufuata msingi wa upangaji matumizi ya Ardhi ambao unazingatia kwenye maeneo yafuatayo:-

- Kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya makazi yenye huduma kwa jamii yote.
- Kuwezesha uboreshaji wa utoaji wa miundombinu na huduma za jamii ili kuwa na makazi endelevu
- Kuwezesha kuwepo fursa za ajira na kuondoa umasikini.

- Kuhimiza uwepo wa mfumo wa ngazi za makazi mizania unaozingatia maendeleo endelevu ya makazi.
- Kuhimiza na kuwepo kwa ushirikishwaji wa sekta binafsi, sekta za umma na taasisi zisizo za kiserikali katika kupanga matumizi ya Ardhi.
- Kulinda mazingira ya makazi ya binadamu na mfumo wa ikolojia dhidi ya uharibifu wa kimazingira ili kufikia maendeleo endelevu.
- Kujenga uwezo wa kitaalamu katika kupanga na kutekeleza mipango ya matumizi ya Ardhi nchini.
- Kujenga uwezo katika ngazi mbalimbali (Kijiji, Wilaya, Kanda, Taifa,) kuhusiana na masuala ya upangaji na usimamizi wa matumizi ya Ardhi.
- Kuakikisha masuala ya Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu pamoja na miongozo mbalilmbali iliyotolewa inafuatwa.

Pia, pamoja na misingi hiyo niliyotaja, madhumuni ya upangaji yanalenga katika maeneo yafuatayo;

- Kuwezesha upangaji wa matumizi ya Ardhi wenye ufanisi na mpangilio unaofaa
- Kuwezesha wamiliki wa Ardhi vijijini na mjini kutumia Ardhi yao vizuri kwa uzajilishaji
- Kuhimiza matumizi ya ardhi endelevu nchini.
- Kuhakikisha kuwepo kwa usalama wa miliki na usawa wa utumiaji rasilimali Ardhi.
- Kuwezesha kuwepo na Mpango wa matumizi ya Ardhi ili kuzuia migogoro ya matumizi ya Ardhi
- Kuwezesha watumiaji wadogo na wakubwa wa Ardhi kwa kuzingatia mahitaji ya kisekta
- Kutoa na kuratibu ushirikano wa kisekta
- Kuhakikisha kuna utashi wa kisiasa na kiutawala katika upangaji wa matumizi ya Ardhi ngazi ya KItaifa, Kanda, wilaya na Vijiji.

Baada ya maelezo hayo napenda pia, kueleza majukumu ya Tume ya kama inavyoelezwa katika Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Sura 116 Kifungu Na. 7. ni;

- Kuratibu, kushauri na kukagua sekta zote kuhusu viwango vya pamoja na kumshauri Waziri kuweka viwango vinavyokubalika;

- Kusaidia mamlaka zote za upangaji wa matumizi ya ardhi kwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi, kufuatilia utekelezaji wake na kuifanyia tathmini mara kwa mara;
- Kuratibu shughuli za vyombo vyote vinavyohusika na mambo ya upangaji wa matumizi ya ardhi kutumika kama njia ya mawasiliano kati ya Taasisi hizo na Serikali;
- Kubuni na kueneza program ambazo zitalinda na kuimarisha kwa ufanisi ubora wa ardhi na upangaji wa matumizi ya ardhi unaofaa;
- Kuhamasisha ushiriki wa umma na sekta binafsi katika shughuli zinazohusiana na upangaji wa matumizi ya ardhi kwa ajili ya matumizi ya ardhi yenye uwiano na manufaa;
- Kuendeleza ushirikiano kati ya Serikali, mamlaka za serikali za mitaa na Taasisi nyingine zinazo jishughulisha na upangaji wa matumizi ya ardhi;
- Kuendeleza maendeleo ya maarifa ya kisayansi katika masuala ya upangaji wa matumizi ya ardhi na kuhimiza maendeleo ya teknolojia yanayolenga uzuiaji au upunguzaji wa madhara makubwa katika ardhi
- Kuanisha viwango, desturi na vigezo kwa ajili ya ulinzi wa matumizi yenye manufaa na kudumisha ubora wa ardhi;
- Kufanya na kuratibu utafiti, uchunguzi na upimaji wa ardhi unaohusiana na upangaji wa matumizi ya ardhi na kukusanya taarifa, kuzipanga kwa utaratibu na kuanzisha benki ya taifa ya takwimu ya kuendeza taarifa kuhusu matokeo ya utafiti, uchunguzi au upimaji wa ardhi nchini;
- Kuanzisha na kuendesha mfumo wa uwekaji, utunzaji kumbukumbu na uenezaji wa taarifa inayohusiana na upangaji wa matumizi ya ardhi;
- Kushauriana na Wizara zote za kisekta, kutathmini sheria zilizopo na kuishauri Serikali juu ya hatua za kisheria na nyinginezo kwa ajili ya upangaji wa matumizi ya ardhi na kupendekeza utekelezaji wake;
- Kuanzisha na kudumisha ushirikiano na nchi nyingine na mashirika ya kimataifa, yanayoshughulikia masuala na mambo yanayohusiana na upangaji wa matumizi ya ardhi;

- Kushirikiana na wakala wanaohusika, kufanya program zinazo kusudia kuimarisha elimu ya upangaji wa matumizi ya ardhi, kuinua mwamko wa umma kuhusu haja ya usimamizi bora wa matumizi ya ardhi na, kushawishi umma kusaidia na kuhimiza jitihada zinazofanywa na vyombo vingine kwa ajili hiyo;
- Kuendesha na kuhamasisha program za mafunzo katika upangaji wa matumizi ya ardhi kwa ajili ya kuelimisha umma juu ya upangaji wa matumizi ya ardhi unaofaa na wajibu wa umma katika ulinzi, matumizi na uboreshaji wake;
- Kuhakikisha utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi iliyoidhinishwa unakuwepo na unafuatwa.
- Kufanya shughuli nyingine kama ilivyoagizwa chini na Sheria husika Sura 116 ya mwaka 2007

Hivyo, kama ilivyo ni takwa la kisheria katika kifungu Na.5 na 6 cha Sura 116 ya Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Tume, ili kutekeleza majukumu yake vizuri, imeamua kurejesha tena kamati ya Taifa ya kiufundi ambayo kwa kushirikiana na sekta husika zinazo jihusisha na uandaaji wa mipango ya matumizi ya Ardhi nchini itapata nafasi ya kujadiliana, kushauriana na Tume kwenye masuala muhimu yafuatayo;

1. Jinsi ya kuanzisha vigezo na taratibu za tathmini ya ubora wa ardhi.
2. Kuweka vigezo vya chini kabisa vya ubora vya ardhi yote ya Tanzania kwa matumizi ya ardhi, ikiwa ni pamoja na:
   a) Ardhi kwa ajili ya matumizi ya kilimo;
   b) Ardhi kwa ajili ya matumizi ya burudani;
   c) Ardhi kwa ajili ya makazi yaliyopimwa;
   d) Ardhi iliyotengwa kwa ajili ya utupaji wa taka;
   e) Ardhi kwa ajili ya matumizi ya wanyamapori;
   f) Ardhi kwa ajili ya misitu ya hifadhi na uzalishaji;
   g) Ardhi kwa ajili ya mifugo na malisho;
   h) Ardhi kwa ajili ya madini na matumizi ya rasilimali za majini; na
   i) Ardhi kwa ajili ya matumizi ya viwanda.

3. Kushari juu ya Miongozo au kanuni za utunzaji wa ardhi endapo ardhi inahitaji uhifadhi maalumu.
4. Kushauri juu ya maeneo ya utafiti kuhusu athari za uchafuzi wa ardhi kwa mazingira, binadamu na wanyama.
5. Kutoa ushari juu ya hatua za lazima za kushughulikia maji machafu kabla hayajatiririshwa kwenye mifereji ya maji machafu.
6. Taratibu za usimamizi wa rasilimali zinazomilikiwa kwa pamoja.
7. Vigezo vya mashauriano na uratibu wa ndani wa sekta.
8. Miongozo ya maamuzi ya pamoja ya wakala wa upangaji kuhusu masuala yenye umuhimu wa pekee.
9. Miongozo ya ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya uidhinishaji.

Baada ya kufafanua masuala ya kuzingatiwa na kamati, naamini kwa muda wa siku tatu tutaeleweshana na kujadiliana zaidi kuhusu mambo yafuatayo;

- Sheria za upangaji wa matumizi ya ardhi.
- Mpango wa Taifa wa matumizi ya Ardhi 2013 – 2033
- Mpango wa matumizi ya Ardhi Kikanda
- Mpango Kiunzi wa Matumizi ya Ardhi ya Wilaya
- Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya kijiji
- Mtizamo wa Mipango Fungamanishi ya Upangaji wa matumizi ya Ardhi, changamoto na mafunzo yaliyopatikana katika kuboresha uandaaji wa matumizi ya Ardhi, Maeneo ya kipaumbele kwenye maeneo ya Upangaji na Usimamizi wa matumizi ya Ardhi.
- Mkakati wa kukabiliana na Changamoto za Mipango ya Matumizi ya Ardhi nchini.
- Mkakati wa Uratibu wa  Tume ya Taifa ya matumizi ya Ardhi
- Mkakati wa Mawasiliano
- Mkakati wa upatikanaji rasilimali

Mwisho nawatakia kheri wanakamati  katika ushirikiano wa kurejesha kamati hii ambayo ni kiungo muhimu katika kuunganisha na kuratibu watumiaji wote wa Ardhi kwa mtazamo au kwa nia ya kuongeza thamani ya Ardhi  na kuhakikisha rasilimali za Ardhi zinatumika ipasavyo na mazingira yanaboreshwa. Pia, nachukua fursa kupongeza wajumbe wote walioteuliwa na taasisi zao kuwa wajumbe wa kamati hii ya kitaifa. Kwa namna ya pekee nachukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza wadau wenzetu wa IUCN na OXFAM kwa kufadhili sehemu ya gharama ya kikao hiki. Aidha nichukue pia fursa hii kuwashukuru wadau wengine wote walioacha kazi zao na kujumuika nasi ambao ni WWF, CARE INTERNATIONAL NA UCRT.

BAADA YA MAELEZO HAYA SASA NINATAMKA KUWA KIKAO CHA KAMATI YA TAIFA YA UFUNDI YA KUPANGA NA KUSIMAMIA MATUMIZI YA ARDHI KIMEFUNGULIWA RASMI NA KAMATI IMEREJESHWA.

ASANTENI KWA KUNISIKILZA.